



Mkopo mpya wa ushuru kwa wafanyakazi wa Washington

Marejesho ya Kodi ya Familia Zilizo na Watu Wanaofanya Kazi yatatoa malipo ya hadi \$1,200 kwa watu binafsi na familia zinazotimiza masharti.

Nani anastahiki kwa marejesho ya kodi?

Familia na watu binafsi wanastahiki ikiwa watatimiza masharti yote yafuatayo:

- Wameishi katika Washington kwa angalau siku 183.
- Wana angalau umri wa miaka 25 na chini ya miaka 65 AU wana mtoto anayetimiza masharti kwa mwaka wa 2022.
- Waliwasilisha ripoti za malipo ya kodi ya nchi ya 2022 kwa Nambari ya Ustawi wa Jamii (SSN, Social Security Number) au Nambari ya Utambulisho ya Mlipakodi Binafsi (ITIN, Individual Taxpayer Identification Number).
- Wanastahiki Marejesho ya Kodi ya Mapato ya nchi kwenye ripoti zao za malipo ya kodi ya 2022.
 - Nenda kwenye www.irs.gov/eitc ili upate maelezo zaidi.
- Wanatimiza masharti ya mapato (angalia jedwali).

Je, familia na watu binafsi watarejeshewa kiasi gani?

Inategemea idadi ya watoto wanaotimiza masharti na kiwango cha mapato. Angalia jedwali kwa makadirio kulingana na viwango vya mapato ya ustahiki vya 2022.

Viwango vya mapato ni gani?

Idadi ya watoto wanaotimiza masharti	Mwombaji lazima awe na mapato ya chini ya viwango vifuatavyo		Marejesho ya juu zaidi
	Wasiofunga ndoa	Waliofunga ndoa (<i>wanaowasilisha ripoti za malipo ya kodi kwa pamoja</i>)	
0	\$16,480	\$22,610	\$300
1	\$43,492	\$49,622	\$600
2	\$49,399	\$55,529	\$900
3 <i>au zaidi</i>	\$53,057	\$59,187	\$1,200

Kipindi cha kutuma maombi kinafunguliwa tarehe 1 Februari 2023 na maombi yatakubaliwa hadi tarehe 31 Desemba 2023.



Ili kupata maelezo ya ziada au kujiandikisha ili kupata taarifa, tembelea tovuti yetu katika:
WorkingFamiliesCredit.wa.gov au piga simu 360-763-7300.